

HALMASHAURI YA WILAYA MLIMBA

SHULE YA SEKONDARI KIBURUBUTU,

S.L.P 287,

IFAKARA,

10/12/2020.

KUMB.MA KSS/F SEL 2020

JINA

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBURUBUTU

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Kiburubutu kidato cha kwanza mwaka 2021. Shule itafunguliwa tarehe 11/1/2021 unapaswa ufike shuleni siku hiyo saa 1:00 Asubuhi.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

(a) Sare ya Wavulana

i. Suruali mbili za rangi ya kijivu

- Iwe na malinda (Celebrations 2) isiyo na malinda haikubaliki.
- Isiwe suruali ya kubana. Iwe suruali ya heshima
- Mshono wa jeans haukubaliki kabisa
- Isiwe na mifuko ya kubandika
- Iwe na mifuko mitatu mbele 2 nyuma mmoja

ii. Mashati mawili meupe tetroni ya mikono mifupi yasiwe ya kubana na yasiwe madogo.

iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu, viwe na kamba. Mabuti na viatu vingine ambavyo havina gidamu havitakubalika.

iv. Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote jozi 2

v. Mkanda wa ngozi mweusi.

(b) Sare ya wasichana

i. Sketi mbili za rangi ya kijivu

- Mshono ni linda box
- Sketi ivuke magoti, sketi fupi haikubaliki

ii. Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule .

iii. Mashati mawili meupe tetroni ya mikoni mifupi yasiwe ya kubana

iv. Viatu vyeupe vya ngozi vyenye gidamu jozi mbili, viatu vya aina nyingine havikubaliki.

v. Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote.

(c) Sare za michezo

Sare ya michezo itahusisha T/Shirt ya shule yenye rangi ya zambarau pamoja na suruali ya shule kwa wavulana na kwa wasichana ni sketi za shule pamoja na T/shirt za shule zenye rangi zambarau

2.2 Vifaa vya masomo

Unatakiwa kuja na Daftari za kutosha (Counter books 11), kalamu na mkebe wa hesabu.

3. 0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya raisi ya TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu, Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kutipoti shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Ni lazima kujisomea wakati wa usiku.
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine unazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa katika maeneo ya shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- (i) Kutunza mali za Umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevywa kama vile uvutaji wa bangi, Cocain, mitungi, kubel n.k
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma
- (g) Kudharau bendera ya taifa
- (h) Kuwa mjamzito au kupata mimba
- (i) Kuoau au kuolewa
- (j) Kutoa mimba
- (k) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (m) Kuwa na simu ya mkononi

4. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni siku ya kuripoti

- (a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu Hospitali ya serikali.

NB: Iwapo mwanafunza amepata shule binafsi toa taarifa ya maandishi kwa mkuu wa shule mapema

KARIBU SANA KIBURUBUTU SHULE YA SEKONDARI

.....
SHABAN A.S NGALAMO

MKUU WA SHULE

0785324642/075812917